

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI**



TAARIFA KWA UMMA

Tunapenda kuutaarifu umma kuwa kuna mtu aliyefungua ukurasa katika mtandao wa kijamii wa 'facebook' kwa kutumia jina la **Mhe. Charles Mwijage**, Waziri wa Viwanda, Biashara na Uwekezaji na kutoa taarifa kuwa Wizara itawapa wananchi pikipiki za bure ili kurahisisha biashara na kupigana na Umasikini.

Wizara inakanusha taarifa hiyo ya kizushi iliyosambaa katika mitandao mbalimbali ya kijamii.

Wizara inachukua hatua za kisheria kuwatambua wale wote waliohusika na kutengeneza ukurasa huo bandia.

Tunatoa wito kwa wahusika wote kuacha maramoja kusambaza taarifa hii potofu.

A handwritten signature in blue ink, appearing to be 'C. Mwijage'.

**IMETOLEWA NA
KITENGO CHA MAWASILIANO SERIKALINI,
WIZARA YA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI**

28 Julai, 2016